BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATOKEO YA SHULE YA SEKONDARI GREEN ACRES

Uongozi wa Baraza la Mitihani la Tanzania unapenda kuujulisha umma kuwa taarifa iliyotolewa katika Gazeti la Tanzania Daima la tarehe **21 Februari 2013** yenye kichwa cha habari "**MATOKEO KIDATO CHA NNE FEKI**" na Gazeti la Mtanzania yenye kichwa cha habari "**MADUDU MATOKEO YA KIDATO CHA NNE**" ni ya upotoshaji na haina ukweli wowote. Katika taarifa hizo imedaiwa kuwa Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari **Green Acres** Ndugu **Julian Bujugo** aliwaeleza Waandishi wa Habari kwamba baadhi ya matokeo ya watahiniwa wa Kidato cha Nne, 2012 yaliyotangazwa tarehe **18 Februari, 2013** yamechakachuliwa. Magazeti hayo yamedai kuwa Ndugu **Bujugo** alieleza yafuatayo kuhusu watahiniwa wa shule ya Sekondari **Green Acres:**

- **S1197/0140 Habib Ibrahim** alifanya mtihani lakini matokeo yake yanaonesha kuwa hakufanya mtihani (Absent); na
- **S1197/148 Humphrey Sanga** hakufanya mtihani lakini amepewa matokeo yakionesha kuwa amefaulu katika kiwango cha daraja la **III** Pointi **24**;
- **S1197/0170 Martin Rushaigo** amepewa matokeo ya masomo ya Biashara ambayo hakuyafanya; na
- **S1197/0172 Mbazi Vota** hakufanya mtihani lakini amepewa matokeo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa kuwa madai yaliyotolewa si sahihi na yanalenga kuchafua hadhi ya Baraza la Mitihani la Tanzania. Ili kuyapa nguvu madai yake Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari **Green Acres** ametumia namba za uongo za watahiniwa kwa lengo la kupotosha umma. Taarifa sahihi za watahiniwa hao ni kama ifuatavyo:

- **S1197/0140 Habib Ibrahim** alifanya mtihani na amepewa matokeo yake.
- **Humphrey Sanga** alisajiliwa kwa namba **S1197/144** na siyo **S1197/0148**. Mtahiniwa **S1197/148** ni **James C. Kaguo**.
- **S1197/172 Mbazi Vota** hakufanya mtihani na hakupewa matokeo.
- **S1197/0170 Martin Rushaigo** hakufanya masomo ya biashara na hana matokeo katika masomo ya biashara.

Fomu ya mahudhurio iliyotumika wakati wa kufanya mtihani inaonesha kuwa watahiniwa **S1197/144 Humprey Sanga na S1197/172 Mbazi Vota** hawakufanya mtihani na Msimamizi amewawekea alama X (Absent) kwenye masomo yote kuonesha kuwa hawakuhudhuria kwenye mtihani. Matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakupewa matokeo na wamewekewa X kwenye masomo yote. Aidha, namba **S1197/0148** ilikuwa ni ya **James C. Kaguo** na amesaini kwenye fomu ya mahudhurio kuthibitisha kuwa alifanya mtihani kwa namba hiyo. Hivyo, matokeo yaliyopo kwenye namba **S1197/0148** ni ya **James C Kaguo** na siyo ya **Humphrey Sanga** kama anavyodai Meneja wa Shule ya Sekondari ya **Green Acres.**

FOMU YA MAHUDHURIO KWENYE MTIHANI SHULE YA GREEN ACRES

September 28, 2012 NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA Page : 997

CSEE 2012 NECTA ENROLMENT LIST FOR : S1197 - GREEN ACRES SECONDARY SCHOOL

CNO	X	CANDIDATE NAME	TOT	011	012	013	014	021	022	024	031	032	033	041	061	062	SIGNATURE
				1	1	1	1 2	1	1	1	1 2	1 2	1 2	1	1	1	
0140	M	HABIB S IBRAHIM	9	✓	✓	✓		✓	✓			✓✓	✓	✓	✓	H.S. Ibrahim	
0144	M	HUMPHREY P SANGA	9	✗	✗	✗		✗	✗			✗✗	✗	✗	✗		
0148	M	JAMES C KAGUO	9	✓	✓	✓		✓	✓		✓✓	✓✓	✓			J.C.Kaguo	
0170	M	MARTIN V RUSHAIGO	9	✓	✓	✓	✓✓	✓	✓			✓✓	✓			M.V.Rushaigo	
0172	M	MBAZI VOTA	7	✗	✗	✗		✗	✗			✗✗	✗				

MATOKEO YA WATAHINIWA HUSIKA KAMA YALIVYOTANGAZWA NA NECTA

CSEE 2012 RESULTS FOR : S1197 - GREEN ACRES SECONDARY SCHOOL

RESULTS SUMMARY
DIV-01 = 0
DIV-02 = 5
DIV-03 = 13
DIV-04 = 98
FAILED = 82

CNO	X	NAMES OF CANDIDATES	PTS	DIV	<--NAMES OF SUBJECTS TAKEN--> CHEMISTRY BIOLOGY KISWAHILI ENGLISH LANGUAGE CIVICS HISTORY GEOGRAPHY BASIC MATHEMATICS COMMERCE
0140	M	HABIB S IBRAHIM	24	III	C D C - D C - - - C D D D
0144	M	HUMPHREY P SANGA	ABS		X X X - X X - - - X X X X
0148	M	JAMES C KAGUO	24	III	D D C - D C - D C C D - -
0170	M	MARTIN V RUSHAIGO	29	IV	D D D F D D F - - D F - -
0172	M	MBAZI VOTA	ABS		X X X - X X - - - X X - -

Baraza la Mitihani linapenda kuwahakikisha wanachi kuwa matokeo ya shule ya Sekondari ya Green Acres yako sahihi kama yalivyotangazwa. Aidha, Baraza la Mitihani limesikitishwa na kitendo cha Mkurugenzi wa Shule ya **Sekondari ya Green Acres** Ndugu **Julian Bujugo** kutoa taarifa za uongo na upotoshaji kwa umma na linawaomba wananchi kupuuza madai hayo ya uzushi.

IMETOLEWA NA:
AFISA HABARI NA UHUSIANO
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA